



## **MTIRIRIKO WA KIKAO CHA BORESHA MAISHA KIDIJITALI**

*Mwongozo huu ukabidhiwe kwa kila Mwenyekiti wa kikundi*

**Zingatia:** Mtiririko huu wa kikao **unatambua kuwa** wanachama wameshajiwekea akiba zao na kulipa mikopo kabla ya kikao kuanza. **Hii inatakiwa kufanyika katika kila mkutano wa Kikundi.**

1. **Mwenyekiti** ahakikishe **ukaaji mzuri** wa wanachama ili kila mmoja **aweze** kushiriki ipasavyo katika **shughuli** zote za kikao. Ni lazima kuhakisha kila mmoja hapati shida ya **kuona** au **kuwasikia** wanachama wengine.
2. Katibu **ahakiki mahudhurio**, kadri itakavyohitajika Mwenyekiti atatakiwa kutoa mwongozo **ilikudhibiti** utoro ambao unaweza kusababisha ugumu wa uendeshaji wa kikao kutokana na **upitishaji** wa maombi.
3. Mwenyekiti **aanzishe ombi la kufungua mkutano**, wanachama wapitishe ombi.
4. Katibu asome **taarifa za shughuli za uwekaji wa Akiba na Taarifa ya Kikundi**
5. Kisha katibu aombe na kusoma **Taarifa ya Hali ya Mikopo**
6. Ikiwa kuna mikopo iliyopita muda wake, **Katibu asome Kumbukumbu za mikopo** hiyo kwa wanachama .
7. Mwenyekiti aongoze mjadala kuhusiana na urejeshwaji wa mikopo yote iliyopita muda wake.
8. Katibu awakumbushe wanachama **Kiasi cha Fedha zilizopo** kwa mujibu wa Taarifa ya Kikundi.
9. Mwenyekiti akaribishe **Maombi mapya ya mikopo** na kuwakumbusha wanaohitaji kukopa kuhakiki **kiasi cha juu cha mkopo kilichopo** kutoka kwenye mfumo wa Boresha Maisha.
  - a. Mwanachama sasa **Ataje kiasi cha Mkopo** anachokihitaji kwa wanakikundi.



- b. Katibu wa Kikundi aorodheshe namba na kiasi cha mkopo cha kila ombi.
  - c. Ikiwa maombi yote yamefanyika, katibu ajumlishe kiasi cha mkopo kinachoombwa kisha alinganishe jumla hiyo na **Akiba ya Fedha Zilizopo**.
  - d. Ikiwa jumla ya maombi ni zaidi ya Fedha zilizopo, Mwenyekiti aongoze mjadala ili kupunguza jumla hiyo. Mapendekezo yaliyopo ni kama ifuatavyo:-
    - i. Baadhi ya wanachama wanaweza kujitolea kusitisha maombi yao.
    - ii. Kikundi kinaweza kujadili upya Madhumuni na “hali ya hatari” ya kila mkopo. Mikopo yenyenye malengo yasiyo ya uzalishaji inaweza kuondolewa na mikopo yenyenye viashiria vya hali ya hatari inaweza kupunguzwa.
    - iii. Mwisho, mikopo yote inaweza kupunguzwa kwa kiasi cha uwiano.
10. Baada ya Jumla ya mwisho iliyombwa na kukubaliwa kuwa ndani ya uwezo wa fedha zilizopo, Mwanachama sasa Aombe Mkopo kwa wanakikundi . Mwenyekiti aongoze mjadala juu ya madhumuni na “hali ya hatari” ya mkopo husika , na athibitishe kiasi ambacho wanakikundi wameridhia kumkopeshwa mwanachama.
11. Katibu **Asajili Mikopo** na wanachama wapitishe ombi la mkopo mmoja baada ya mwingine.
12. Ikiwa kuna jambo lolote la **dharura** lifanyiwe kazi na kukamilishwa.
13. Mwenyekiti aombe **kufunga mkutano**, na wanachama wapitishe ombi.
14. Mwenyekiti awakumbushe wanachama **siku na muda** wa mkutano ujao.

